



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

**Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:**

Tel: +255 262 965732 (Direct line)

+255 659 566703

e-mail: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

Tovuti: [sikongedc.go.tz](http://sikongedc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

4 Mtaa wa Bomani

S.L.P 70

45382 - SIKONGE TABORA

7/06/2023

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUKODISHA CANTEEN (MGAHAWA)  
MPYA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA YA CHAKULA ILIYOPO  
KWENYE JENGO LA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI –  
LGA/121/2023/2024/NC/03**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anawatangazia Wazabuni /Makampuni / Wajasiliamali / Ushirika / Vikundi au Wananchi wenye uwezo wa kukodi Canteen mpya kwa ajili ya kutoa huduma ya Chakula iliyopo kwenye jengo la Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge .

**MASHARTI YA MWOMBAJI.**

1. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania
2. Mwombaji aambatishe kivuli cha Leseni ya Biashara
3. Mwombaji aambatishe kivuli cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN) number
4. Mwombaji aambatishe kivuli cha taarifa za Kampuni (**Company Profile** kwa makampuni tu)
5. Awe amesajiliwa na GPSA kwa mkataba wa '**FOOD AND REFRESHMENTS**'
6. Mwombaji ataje kiasi cha fedha atakacholipa Halmashauri kwa mwezi (Malipo ya pango kwa mwezi) na malipo haya yatafanyika kila mwanzo wa mwezi (kabla ya kuanza kazi) katika mwezi husika kwa kuchukua 'Control number' toka Ofisi ya Idara ya Fedha
7. Mwombaji atakayepata kazi hii atawajibika kulipia bili ya umeme na maji kulingana na atakavyoelekezwa na Halmashauri
8. Gharama za Usafi kwenye eneo la biashara ni jukumu lake mwenyewe
9. Mwombaji awe na vyombo vya kutosha kufanyia kazi


10. Mwombaji awe na vitendea kazi mwenyewe kama viti, meza, kabati za kuhifadha chakula nk.
11. Mwombaji ataje uzoefu na sifa zake zote katika maombi ya kazi anayoomba
12. Endapo Mwajili hataridhika na mwenendo wa huduma inayotolewa na Mzabuni atasitisha mkataba wakati wowote.
13. Mwombaji atakayepata kazi hii ahakikishe Wafanyakazi wake wana vyeti vya kupima Afya (Medical Examination Certificate).

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA NI KAMA IFUATAVYO;**

- i. Mwaombaji anatakiwa kulipia Kitabu cha Zabuni kwa kazi aliyoomba kiasi cha Tsh. 30,000/= baada ya kupewa Bill / Control number / Account number toka Ofisi ya Mwekahazina / Uhasibu. Kitabu cha zabuni kinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU). **Risiti original aliyolipia mwombaji iambatanishwe kwenye barua yake ya maombi.**
  - ii. Mwombaji aandike jina na namba ya kazi aliyoomba juu ya bahasha ya maombi na atatoa **NAKALA MOJA** ya kitabu cha maombi na kitabu kimoja **ORIGINAL** vyote vifungwe kwenye bahasha moja na kuandikwa **JINA na NAMBA YA ZABUNI** husika juu ya bahasha ya maombi
  - iii. Barua ya Maombi iandikwe kwenda anwani ifuatayo;  
**KATIBU BODI YA ZABUNI,**  
**S.L.P 70,**  
**SIKONGE.**
  - iv. Vigezo vya tathimini ya zabuni hii ni kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya manunuzi ya umma 2011 na kanuni zake 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016
14. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni tarehe 20/06/2023, Jumanne saa 5.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

Waombaji au Wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa maombi yao. Baada ya ufunguzi taratibu zingine za Manunuzi zitafuata.

Imetolewa na;

  
Seleman M. Pandawe  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**SIKONGE**

2

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**WILAYA - SIKONGE**